HALMASHAURI YA WILAYA YA MONDULI
MKOA WA ARUSHA
Barua zote ziandikwe kwa mkuu wa shule
Simu: 0757404987/0655055204
Email:nanjasekondari@gmail.com
SHULE YA SEKONDARI NANJA
S.L.P 37
MONDULI.
ARUSHA - TANZANIA.
EDUCATION FOR EXCELLENCE CHANGE

TAREHE: .....

Kumb. Na: MOND/NANJA/SS//JOIN/2024/05

JINA LA MWANAFUNZI……..

SHULE YA MSINGI ATOKAKO……

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NANJA WILAYA YA MONDULI MKOA ARUSHA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2024

1. UTANGULIZI

Ninafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga Kidato cha Kwanza mwaka 2024 katika Shule ya Sekondari **NANJA**. Shule ya Sekondari Nanja ipo Mkoa wa **Arusha** Wilaya ya **Monduli** Kata ya **Sepeko**, umbali wa **km 35** kutoka makao makuu ya Wilaya barabara kuu ya kutoka **Duka Bovu - Makuyuni/Karatu.** Usafiri wa basi kutoka Monduli mjini unapatikana katika kituo cha mabasi cha Monduli nauli ni **Tsh 3,000/=.** Kwa wale wa karibu wanaweza kufika kwa miguu kwani shule ipo karibu na barabara kuu.

Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe **08/01/2024**, unatakiwa kufika shuleni kuanzia tarehe **08/01/2024** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **22/01/2024** ndani ya siku **14**, tangu shule ilipofunguliwa. Mwanafuzi asiporipoti shuleni hadi kufikia tarehe **22/01/2024** mzazi atakamatwa na kushitakiwa kwa kosa la kumnyima mtoto haki ya kusoma.

Muhimu:

1. Mwanafunzi aweke alama kwenye sare yake ya shule ili kupunguza wizi
2. Hakikisha sare zinafanana na sampuli iliyoambatanishwa na fomu hii ili kuepuka usumbufu, aidha soma maelekezo yote kwa umakini na fomu zote zijazwe kisha zirudishwe shuleni.
3. Fomu hii ni batili kama haina muhuri **"ORIGINAL"** wa mkuu wa shule na sampuli za vitambaa vilivyoambatanishwa. Hairuhusiwi kutoa **Nakala (copy)** fomu hii ili kuepuka kupata fomu isiyo na sampuli ya vitambaa vya sare za shule.
4. Njoo na fomu hii ikiwa **HALISI** (Original) na ikiwa imejazwa vizuri fomu zote.
5. Fomu ya Daktari ijazwe na daktari aliyeidhinishwa katika hospitali ya Serikali baada ya mtoto kupimwa
6. Mwanafunzi asipofika shuleni ndani ya siku 14 mzazi atakamatwa na kushtakiwa.
7. Siku ya kuwaona watoto ni siku zote za Juma na wanaoruhusiwa kuwatembelea wanafunzi ni mzazi/mlezi halisi aliyeandikishwa shuleni tu. Fika ongea na mwanao si zaidi ya dakika kumi kisha urudi nyumbani. **Kama kuna ndugu au rafiki aambatane na mzazi wa mwanafunzi asije mwenyewe.**

2. MAHITAJI YA MWANAFUNZI.

SARE ZA SHULE

A. WAVULANA

i. Suruali mbili za heshima (suruali ziwe ndefu ziguse kwenye viatu na ziwe na marinda 2) zisibane yaani zisiwe "mnyonyo" Rangi ya **KIJANI mpauko (rangi ya choroko) grade 1 - one** isiyopauka kama sampuli ya kitambaa kilichoambatanishwa
ii. Mashati mawili meupe ya mikono mifupi
iii. Sweta rangi **NYEKUNDU** shingo ya V na mkanda mweupe shingoni na mikononi. Rangi ya uzi imeambatanishwa.
iv. Soksi nyeusi jozi mbili
v. Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga kamba visivyochongoka
vi. Mkanda wa ngozi mweusi, usio na urembo
vii. Suruali **NYEKUNDU DAMU YA MZEE** kwa ajili ya kushindia (kitambaa kimeambatanishwa)
viii. T.shirt rangi **NYEKUNDU aina ya tetroni** kama rangi ya sweta kwa ajili ya kushindia. Isiwe mtumba na isiyo na maandishi yoyote
ix. Traki suti rangi **NYEKUNDU** kwa ajili ya kushindia na usiku wakati wa kujisomea

B. WASICHANA

i. Sketi mbili za marinda 8 za heshima (urefu uwe katikati ya magoti na kisigino) rangi ya **Kijani Mpauko (rangi ya choroko) grade 1 (one)** isiyopauka kama sampuli ya kitambaa kilichoambatanishwa
ii. Shati mbili nyeupe mikono mifupi
iii. Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga kamba visivyo na visigino virefu (viatu maarufu kama bajaji haviruhusiwi kabisa)
iv. Sweta rangi **NYEKUNDU** shingo ya V yenye mkanda mweupe shingoni na mikononi, uzi umeambatanishwa.
v. Soksi ndefu nyeupe jozi mbili
vi. Sketi ya rangi **NYEKUNDU DAMU YA MZEE** kwa ajili ya kushindia- shamba dress (kitambaa kimeambatanishwa)
vii. T.shirt rangi **NYEKUNDU aina ya tetroni** kama rangi ya sweta kwa ajili ya kushindia. Isiwe mtumba na isiyo na maandishi yoyote
viii. Traki suti ya rangi **NYEKUNDU** kwa ajili ya kushindia na usiku wakati wa kujisomea
ix. Hijab Nyeupe siyo kilemba au mtandio (kwa Waislamu tu)
x. Taulo za kike (Pedi) za kutosha na mahitaji mengine muhimu kwa mtoto wa kike.

NGUO NYINGINE ZOTE ZA NYUMBANI HAZIRUHUSIWI KABISA. UKIJA NAZO UTANYANG'ANYWA NA ZITACHOMWA MOTO

3. VIFAA BINAFSI VYA MWANAFUNZI KWA WOTE

i. Godoro moja la inchi mbili na nusu ($2^1/_2$x6) godoro la"TANFOAM" Original liwe na kitambaa (cover) godoro original linakuwa na muhuri wa moto. Ukinunua godoro imara (original) utaepuka usumbufu wa kununua godoro mara kwa mara kwani litadumu kwa miaka mingi kuliko godoro feki.
ii. Blanketi 1 rangi yoyote
iii. Shuka mbili rangi ya pinki
iv. Ndoo ndogo moja ya lita 10
v. Sanduku la Bati ukubwa wa wastani lenye kufuli imara.
vi. Vyombo vya chakula kama Sahani, bakuli, kikombe na kijiko. Hakuna mwanafunzi atakayeruhusiwa kushiriki chombo cha chakula na mwenzake.
vii. Aje na jembe lililonolewa na kuwekwa mpini vizuri kwajili ya kuotesha miti na bustani kwa ajili ya somo la kilimo.
viii. Begi imara (school bag) kwa ajili ya kubebea vitabu na daftari
ix. Ream moja A4 kwa ajili ya kufanyia mitihani na mazoezi ya mara kwa mara hapa shuleni.
x. Daftari kubwa 10 (counter book Quire3), kalamu, penseli, mkebe. Madaftari yajaladiwe.
xi. Kamusi ya kingereza kwa kingereza (Oxford Dictionary) kwa ajili ya kumsaidia kumudu lugha ya kingereza
xii. Vifaa vya michezo kama vile bukta, raba, t-shirt, Vyote viwe na rangi **NYEKUNDU**. Atatumia siku za michezo tu.
xiii. Rain boot (buti kwa ajili ya matope) kipindi cha mvua
xiv. Aje na kiasi cha Tsh. 5,000/- kwa ajili ya kukata bima ya afya. Kwa wale wenye bima yeyote ya Afya waje nazo badala ya fedha zilizotajwa.
xv. Aje na kitabu kimoja cha somo lolote kidato cha kwanza.
xvi. Aje na karatasi laini (toilet paper) pc 4 kwajili ya kutumia chooni.

Karibu sana Shule ya Sekondari Nanja.

…….
SADOTH P. RUTAYUGA
MKUU WA SHULE
0757404987

4. SHERIA NA KANUNI ZA SHULE.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa **sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978** na kama ilivyorekebishwa kwa **sheria Na. 10 ya mwaka 1995**. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na mafunzo ya usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

a. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima
b. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima
c. Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
d. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazoagizwa.
e. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii
f. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule
g. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
h. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
i. Kutunza mali za umma

MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUKUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE.

a. Wizi
b. Uasherati na ushoga
c. Ubakaji
d. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kuberi n.k
e. Kupigana au kupiga
f. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
g. Kudharau mawala ya kitaifa kama vile bendera ya Taifa, wimbo wa Taifa n.k
h. Kuwa mjamzito/ kupata mimba/kutoa mimba/kumpa mwanafunzi mimba
i. Kuoa au kuolewa
j. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
k. Kukataa adhabu kwa makusudi
l. Kumiliki simu ya mkononi
m. Kuwekwa /kuweka kimada
n. Kuzurura ovyo kwenye nyumba za walimu

……
SADOTH P. RUTAYUGA
MKUU WA SHULE
0757404987

5. FOMU MAALUMU YA TAARIFA MUHIMU KUHUSU MWANAFUNZI

Toa taarifa zifuatazo bila kuogopa na bila kushawishiwa na mtu yeyote

i. TAJA JINA LAKO KAMILI ……
ii. TAREHE YA KUZALIWA……..
iii. UMRI……
iv. MAHALI PA KUZALIWA……...
v. URAIA……..
vi. JINSIA (ME/KE)……...
vii. DINI……..
viii. KABILA LAKO……
ix. MAHALI WANAKOISHI WAZAZI WAKO (kitongoji/kijiji/kata)…….……..
……
x. SHULE YA MSINGI ULIYOSOMA …….
xi. JE ULIANZA DARASA LA KWANZA KWENYE SHULE ULIKOMALIZA DRS LA 7 AU ULIHAMIA ?……..……..…KAMA ULIHAMIA, ULIHAMIA KUTOKA SHULE GANI…….....
xii. UNAISHI NA WAZAZI WAKO WOTE? TIKI KI MOJAWAPO
a) Naishi na wazazi wote wawili ☐ b) Naishi na baba tu ☐ c) Naishi na mama tu ☐ d) Wazazi wangu wote hawapo hai. Hivyo naishi na ndugu wengine ☐
e) Taja jina la mtu unayeishinaye ……..…… f) mahusiano……
xiii. TAJA CHAMA, SHIRIKA, KIKUNDI CHA DINI AU JUMUIYA INAYOKUFADHILI KAMA IPO……..
xiv. KATIKA MAISHA YAKO UNGEPENDA KUSOMA MASOMO GANI KATI YA SAYANSI,KILIMO NA SANAA (arts) ? …….
xv. KATIKA MAISHA YAKO UNGEPENDA KUWA NANI? (mfano, daktari wa binadamu, mwalimu, mhandisi wa ujenzi, mwandishi wa habari, rubani, nahodha, daktari wa mifugo,Aisa kilimo, afisa wanyama pori nk)……
xvi. TAJA KARAMA YAKO (TALENTS) YAANI KITU ULICHONACHO YA KIPEKEE KATIKA MAISHA YAKO (mfano mcheshi, mchekeshaji, mchezaji wa mpira wa miguu au netball, mwaandishi wa habari,nk)……

xvii. ORODHESHA MICHEZO UNAYOPENDA UKIANZIA NA ULE UNAOPENDA ZAIDI
a)……..
b)……..
c)…….
xviii. TAJA NDUNGU ZAKO WAWILI WA KARIBU AMBAO WANAWEZA KUKUTEMBELEA SHULENI
(1)…… (2)……...……..
xix. NYUMBANI KWENU KUNA NDUGU ZAKO WALIOWAHI KUSOMA SEKONDARI?
……
xx. JE UMEWAHI KUOTESHA MTI? .....
xxi. JE UNAPENDA MAZINGIRA? ……NA UNGEPENDA KUPEWA MTI WA KUTUNZA UKIFIKA SHULENI? …….
xxii. KAMA USINGECHAGULIWA KUJIUNGA NA SEKONDARI UNGECHUKUA HATUA GANI KUHAHIKISHA UNASOMA ELIMU YA SEKONDARI?
.....

6. MAWASILIANO:

Namba za shule kwajili ya mawasiliano angalia nembo ya shule kwenye fomu hii utazipata. Fomu hii inakuhitaji mzazi utaje majina ya viongozi wa kitongoji/ kijiji na mawasiliano ya wazazi pamoja na namba zao za simu. Hakikisha unajaza namba sahihi na endapo kutakuwa na mabadiliko hakikisha unampa mwanao namba mpya zilizobadilika ili kwa namna yeyote tusikose mawasiliano yako.

1. Jina la Mwenyekiti wa serikali ya kijiji au kitongoji au Mtaa utokako……..……..……
Namba ya simu ya mwenyekiti wa kijiji/kitongoji/mtaa……
2. Jina la Balozi wa mtaa…….……..……..…....
Namba ya simu ya Balozi……..
3. Jina la baba/mlezi……..……..…..……....
Namba ya simu…….……...……..
4. Jina la mama/mlezi……
Namba ya simu……..…
5. **Taja Ndugu wawili wa karibu:**
    1. Jina…….……Namba za simu…….……..
    2. Jina…….Namba za simu ……..

7. UTHIBITISHO WA MWANAFUNZI KUSOMA NANJA SEKONDARI.

Mimi …… (Jina la mwanafunzi) Ninathibitisha kuwa taarifa nilizojaza hapo juu ni sahihi na nakubaliana na sheria, kanuni na taratibu zote za shule. Ninaahidi kuwa Mtiifu kwa muda wote nitakapokuwa shuleni na endapo nitakiuka sheria, kanuni na taratibu za shule niko tayari kuadhibiwa kulingana na taratibu za shule.

Jina kamili la mwanafunzi……. saini……...tarehe…….……
Jina la mzazi/mlezi……..…….Saini……..…...…tarehe……
Uthibitisho wa mwalimu wa Usajili/Nidhamu shule ya Sekondari Nanja
……
……
Saini ……..…….....tarehe……..

8. AHADI YA MZAZI/MLEZI KUHUSU MALEZI YA MWANAWE

(ijazwe na mzazi /mlezi wa mwanafunzi na kuiwasilisha shuleni)

Mimi…… ambaye ni mzazi /mlezi wa mwanafunzi ……..……
Ninaahidi kumhudumia mwanangu na kumpatia mahitaji yake kwa wakati na kushirikiana na shule kumlea mtoto huyu. Aidha ninaahidi kwamba nitahakikisha mwanangu anasoma na kuhitimu kidato cha nne na hivyo sitakubaliana na utoro wa aina yoyote. Nitashirikiana na uongozi wa shule kuhakikisha mwanangu wa **KIKE** hatapata **UJAUZITO** wala sitamwoza au kupokea mahari wakati wote wa masomo yake. Endapo nitakiuka ahadi hii hatua kali za kisheria zichukuliwe dhidi yangu.

Saini ya mzazi……tarehe……simu…….

HALMASHAURI YA WILAYA YA MONDULI
MKOA WA ARUSHA
Barua zote ziandikwe kwa
mkuu wa shule
Simu: 0757404987/0655055204
Email:nanjasekondari@gmail.com
SHULE YA SEKONDARI NANJA
S.L.P 37
MONDULI.
ARUSHA - TANZANIA.
EDUCATION FOR EXCELLENCE CHANGE

Ref: No. **MOND/NANJA/SS//JOIN/2024/05**
(**PART A :**)
MEDICAL OFFICER ……..

RE: REQUEST FOR EXAMINATION TO ……
Please examine the above named as his/her physical and mental fitness for full time schooling course. The examination should include the following categories (i – iii) each category or sub category of which will render ineligible in case of defect. Pregnancy (category viii) will also render a girl candidate ineligible to the course

……
THE HEAD MASTER

PART B
MEDICAL CERTIFICATE

(To be completed by Government Medical Officer)
I have examined the above named and consider that he/she is physically fit/ unfit and mentally fit/ unfit for full time schooling course

PHYSICAL HEALTH

i. Eye ……..
ii. Hearing ……..
iii. Limbs …….
iv. Leprosy ……..
v. Epilepsy…….
vi. Neuroses ……
vii. Other serious diseases ……
viii. Pregnancy …….
ix. Any other comments regarding your examination …….....
……

Station …….. Designation……..
Signature (Official Stamp) ……..…… Date …….……